**Learning on TAP**

# Teknolojia saidizi

Jumbe muhimu: Vifaa saidizi vya usikivu vinavyoweza kusetiwa

## Somo la kwanza 1: Utangulizi wa vifaa saidizi vya usikivu vinavyoweza kusetiwa

Moduli hii imetengenezwa kutoka kwenye moduli ya TAP inayohusu vifaa saidizi vya usikivu vilivyosetiwa tayari kwa kutoa vifaa saidizi ya kusikia vinavyoweza kusetiwa vya watoto.

### Matokeo ya vifaa saidizi vya usikivu kwa watoto.

Vifaa saidizi vya usikivu vinawasaidia watoto waliopoteza usikivu kuweza kusikiliza mazungumzo na sauti katika mazingira yao. Vifaa saidizi vya usikivu vinaweza kupunguza madhara ya kupotea kwa usikivu. Vinamsadia mtoto katika kujifunza kwake shuleni, kuwasiliana na watu pamoja na kutengeneza urafiki, mazungumzo na kujenga uwezo wa kumudu lugha.

### Tathmini ya vifaa saidizi vya usikivu


Watoto wenye umri wa miaka mitano au zaidi wanaweza kutathminiwa na kutafutiwa kipimo sahihi cha vifaa saidizi vya usikivu vinavyoweza kusetiwa. Watoto walio na umri chini ya miaka 5 wanaweza pia kutumia vifaa saidizi vya usikivu vinavyoweza kusetiwa. Hatahivyo, wanaweza kuhitaji kufanyiwa tathmini na mtu ambaye amepata mafunzo zaidi ☞ Mpe rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu

Tathmini ya vifaa saidizi vya usikivu inahitaji kipimo cha usikivu. Kabla ya kufanya kipimo cha usikivu kagua afya ya masikio ili kujua kama masikio yote mawili yana afya bora. Matokeo ya kipimo cha usikivu wa mtoto yanaweza kuweka katika viwango sita tofauti kwa kila sikio. Viwango hivi vinatokana na wastani wa kiwango cha chini kabisa cha sauti ambacho kinaweza kusikika kwa kila sikio.

| Viwango vya kupotea kwa usikivu | Mapendekezo |
|---|---|
| 1. Usikivu wa kawaida<br>2. Upotevu kidogo wa usikivu<br>3. Upotevu kiasi wa usikivu<br>4. Upotevu mwingi kiasi wa usikivu<br>5. Upotevu mkubwa wa kiwango cha kusikia<br>6. Upotevu kiasi kikubwa sana cha usikivu | Watoto waliopoteza usikivu kwa kiwango kidogo hadi kiwango kikubwa wanashauriwa kutumia vifaa saidizi vya usikivu.<br>Watoto waliopoteza usikivu kwa kiwango kikubwa hadi kwa kiwango kikubwa zaidi wana mahitaji mengi na wanapaswa ☞ kupewa rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu |

### Vifaa saidizi vya usikivu vinavyoweza kusetiwa

Iwapo mtoto amepoteza usikivu anashauriwa kutumia vifaa saidizi vya usikivu kwa masikio yote mawili. Vifaa hivi vyaweza pia kutumiwa na watu wazima. Kama mtu mzima anahitaji vifaa saidizi vya usikivu vinavyoweza kusetiwa ☞ apewe rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu.



**Marekebisho ya vifaa saidizi vya usikivu vinavyoweza kusetiwa:**

Vifaa saidizi vya usikivu vinarekebishwa kwendana na mahitaji binafsi.

Vinaweza kurekebishwa kwa:

- Kutumia programu iliyoko kwenye kompyuta.
- Apu

Vinatoa sifa za ziada ili kuifanya sauti iwe nzuri zaidi.

## Somo la 2: Hatua ya kwanza: Chagua

### Mambo ya msingi kuhusu tathmini.

Kupitia tathamini utapata taarifa kuhusu uwezo wa mtoto kusikia na kiwango cha kupotea kwa usikivu alichonacho. Taarifa hii itakusaidia pamoja na mlezi wake kuweka mpango wa utatuzi wa tatizo.

- Kujua kama anaweza kufaidika na matumizi ya vifaa saidizi vya usikivu.
- Aina ya vifaa saidizi vya usikivu ambavyo vinafaa.
- Mambo ya kufundisha
- Ufuatiliaji
- Rufaa kwenda kwenye huduma nyingine.

Kama mtoto tayari ana vifaa saidizi vya usikivu na anarudi kwenye huduma, tathmini hii itasaidia kujua kama vifaa saidizi vya usikivu vinatakidhi mahitaji yake.

### Maandalizi ya kipimo cha usikivu

Kabla ya kufanya kipimo cha usikivu, hakikisha mazingira yanafaa kwa ajili ya upimaji kwa kupima kiwango cha kelele kutoka nje ya eneo la upimaji. Kiwango cha kelele kutoka nje ya eneo la upimaji kinapaswa kuwa pungufu ya desibeli (dB) 40.



Mtayarishe mtoto kwa kumwelezea kuwa kipimo ni rahisi, kinafurahisha na kinafanyika katika njia ya kama mchezo. Maelezo haya yanapaswa kwendana na umri wa mtoto. Onyesha kifaa ili ajue kile kitakachofanyika wakati wa kipimo cha usikivu. Mhusishe mtoto na mlezi

### Kipimo cha usikivu

1. Elezea kipimo cha usikivu
2. Fanya mazoezi ya utoaji majibu ya kipimo. Kama mtoto hafaulu kipimo, usiendelee na kipimo cha usikivu.
3. Fanya kipimo cha usikivu. Mtoto anapaswa kujibu vizuri walau mara mbii kati ya mara tatu ili kuthibitisha kiwango cha chini cha sauti ambacho kinaweza kusikika kwa kila masafa.
4. Kokotoa wastani wa kiwango cha chini kabisa cha sauti ambacho kinaweza kusikika. Tofauti kati ya sikio  la kulia na kushoto inapaswa kuwa pungufu ya dB 15.
5. Rekodi matokeo ya kila sikio. Jumuisha hali ya kujiamini na kiwango cha usikivu uliopotea kwa sikio la kulia na la kushoto.

**Dondoo**
Kama mtoto hatoi majibu mazuri anapopimwa, jaribu: kubadiisha ishara ya majibu, kwa kutumia midoli mhamasishe au muombe mlezi au mtoto mwingine kumwelekeza kwa kutumia vitendo.

### Weka mpango

- **Simamia:** Weka mpango wa ufuatiliaji ndani ya mwaka mmoja kwa watu wazima ambao wana upotevu wa kiwango cha kusikia kuanzia hali ya kawaida hadi kiasi, na pima usikivu kwa mara nyingine.
- **Toa rufaa:** Kwa ruhusa ya mgonjwa, mpe rufaa mgonjwa mtu mzima mwenye upotevu wa usikivu kwa kiwango kiwango zaidi ya dB 15 kama tofauti ya wastani wa kiwango cha chini kabisa ambacho mgonjwa anaweza kusikia kati ya sikio la kulia na kushoto; Aende kwa mtaalamu wa masikio na usikivu.

Baadhi ya watu wanaweza kufaidika na vifaa saidizi vya usikivu. Mtu anaweza kuhitaji muda kufikiria kama wanahitaji vifaa saidizi vya usikivu. Elezea faida za kutumia vifaa saidizi vy akusika na wape fursa ya kufanya mazoezi kwa utumia kifaa saidizi cha usikivu kabla hawajaamua.

- **Chagua** aina ya vifaa saidizi vya usikivu, ukubwa sahihi wa sehemu ya vifaa saidizi inayowekwa kwenye mfereji wa sikio na betri. Weka kumbukumbu.
- **Fundisha** namna ya kutumia  ili mtumiaji aweze kufaidika na vifaa hivi kwa kiwango kikubwa.
- **Ufuatiliaji** ndani ya wiki mbili kuangalia namna mtumiaji anavyoendelea na utumiaji wa vifaa hivi.

## Somo la 3: Hatua ya pili: Kipimo sahihi

### Kagua kifaa saidizi

Kabla ya kutafuta kipimo sahihi cha kifaa saidizi, kagua kifaa saidizi cha usikivu kama hakina dalili zozote za kuharibika na kinafanya kazi vizuri. Unapaswa kusikia vizuri sauti zote za Lingi

### Kupanga programu

Kupanga programu za kifaa saidizi cha usikivu kutasaidia kurekebisha kiwango cha sauti kwendana na matokeo ya kipimo cha usikivu. Kabla ya kuanza, hakikisha programu ya kifaa saidizi cha usikivu au apu imepakuliwa kwenye kifaa chako na kifaa saidizi cha usikivu kimeunganishwa. (namba maalum ya utambulisho inapaswa kuonekana)

- Tengeneza rekodi kwa kutumia maelezo ya mtoto na matokeo ya kipimo cha kusikia.
- Andika aina ya kifinyazi cha kusikia. Chagua fomula inayoelekeza ( hii imetengenezwa moja kwa moja kwenye kifaa) ili kuweka programu kwenye kifaa saidizi cha usikivu kwa kutumia mipangilio inayofaa saizi kwa mtoto. Chagua “kipimo sahihi kwanza” na sevu mipangilio kabla ya kufunga apu na kutenganisha kifaa saidizi na kifaa kinachoweka programu.

### Vifaa saidizi vya usikivu vya majaribio

Baada ya kupangilia vifaa saidi vya kusikia, ni muhimu kufanya majaribio ya vifaa saidizi vya usikivu. Jaribio la vifaa saidizi vya usikivu vitajumuisha:

- Kutafuta kipimo sahihi cha vifaa saidizi vya usikivu.
- Kurekebisha vifaa saidizi vya usikivu

### Kutafuta kipimo sahihi cha vifaa saidizi vya usikivu

Anza kwa kutafuta kipimo sahihi cha kifinyazi cha sikio. Kifaa hiki kinapaswa kumfanya mtumiaji kujisikia vizuri na kuvaliwa/ kuvuliwa kutoka kwenye mfereji wa sikio kwa urahisi.

Kupunguza urefu wa bomba la sehemu ya kifaa saidizi na kupata urefu unahitajika. Bomba linakuwa na urefu sahihi pale kifaa saidizi cha usikivu kinavyokaa vizuri juu ya sikio la mtumiaji bila ya kuacha nafasi.

### Kurekebisha vifaa saidizi vya usikivu



Hakiki kama mtoto anaseikia sauti yako vizuri anapokuwa amevaa vifaa saidizi ya kusikia

1. Kutumia kipimo cha sauti za Lingi. Sauti zinatumika kuwakilisha sauti kwenye masafa ya chini, kati na ya juu. Kama mtoto anajibu kwa sauti zote sita za Lingi, inaonyesha kuwa anaweza kusikia mazunguzo katika kiwango cha kaiwada cha maongezi. Mtoto anapaswa kusikia walau sauti tano kati ya sita ili kufaulu kipimo.
2. Kagua mwangwi wa kifaa saidizi cha kusikia. Haupaswi kuwa na mwangwi ( sauti ya mluzi),
3. Muulize mtoto na/au mlezi maswali ili kujua kama mtoot anajisikia vizuri anapotumia vifaa saidizi vya usikivu vyake. Virekebishe kama itahitajika.
4. Kama mtoto na mlezi wake hawajaridhika na majaribio, jadiliana na mshauri wako. ☞ Toa rufaa kwenda kwa mtaalamu wa masikio na usikivu kama itahitajika.

## Somo la 4: Hatua ya tatu: Matumizi

### Namna ya kutumia vifaa saidizi vya usikivu

Ni muhimu kuelezea faida za kutumia kifaa saidizi cha usikivu na kuhamasisha wahitaji kuwa na mazoea ya kuvitumia mara kwa mara wakati wanasikiliza sauti zao wenyewe na sauti nyingine.

Mfundishe mtumiaji namna ya kutumia kifaa saidizi cha usikivu vizuri ikiwemo namna ya:

- Kutambua sehemu za kifaa saidizi cha kusikia.
- Kuwasha na kuzima kifaa saidizi cha kusikia
- Kurekebisha sauti ya kifaa saidizi cha kusikia
- Kuvaa na kuvua kifaa saidizi chake cha kusikia
- Kuondoa na kutunza betri

### Namna ya kutunza vifaa saidizi vya usikivu.

Ili kuzuia uharibifu, ni muhimu kumfundisha mtumiaji namna ya kutunza vifaa saidizi vyake vya kusikia. Hii ni pamoja na:

- **Kusafisha sehemu ya kifinyazi cha sikio:** sehemu ya kifaa saidizi inayochomekwa kwenye mfereji wa sikio tu, ndio inapaswa kusafishwa na maji!
- **Epuka uharibifu kutokana na maji:** Ni muhimu kulinda kifaa saidizi cha usikivu dhidi ya kupata maji.
- **Kukitunza kwa usalama:** Epuka unyevu kwa kikipangusa kila siku. Wakati wa kwenda kulala kihifadhhi kwenye kifaa cha kuondoa unyevu usiku mzima . Tunza betri kwenye boksi ya kifaa saidizi cha kusikia

## Somo la 5: Hatua ya nne: Ufuatiliaji

### Ufuatiliaji wa kifaa saidizi cha usikivu kwa watoto

Ufuatiliaji wa watoto unahusisha watoto wenye umri kati ya miaka 5-17. Inashauriwa ufuatiliaji wa mapema kwa wiki mbili na miezi miwili ili kumsaidia mtumiaji kurekebisha kifaa saidizi chake na kuweza kupata faida kubwa kutokana na utumiaji huo.

Watoto wanaweza kusababisha kuchakaa kwa vifaa saidizi vya usikivu. Inashauriwa kufanya ufuatiliaji wa vifaa saidizi baada ya miezi sita . Muombe mlezi kuleta vifaa saidizi vya usikivu kituoni ili vifanyiwe ukarabati na kukaguliwa.

Kutathmini kwa mara nyingine ni muhimu kwa watoto kila baada ya mwaka mmoja,Mahitaji yao yanaweza kubadilika haraka kulika watu wazima kwa vile bado wanakua. Ufuatiliaji unaweza kufanyika mtu akiwa mbali kwa njia ya simu au simu ya mnato au mtu kufika kituoni. Miadi ya kutathmini kwa mara nyingine inapaswa kufanyika **mtumiaji wa kifaa akiwepo kituoni na wala si kwa njia ya simu**

- Ufuatiliaji wa vifaa saidizi cha kusikia utakusaidia kujua kama:
- Vifaa saidizi vinakidhi mahitaji ya mtumiaji
- Vifaa saidizi vinahitaji kurekebishwa au kubadilishwa
- Bado vifaa saidizi vinamtosha vizuri mtumiaji.
- Mtoto anahitaji kujua mbinu ya kutatua matatizo na matumizi sahihi

### Faida za kutumia vifaa saidizi vya usikivu

Ili kujua kama mtoto anafaidika na vifaa hivi, angalia kama:

- Wanaridhika na namna wanavyohisi na uzoefu wao wa kutumia vifaa hivi
- Wanatumia vifaa saidizi vya usikivu zaidi ya masaa manne kwa siku.

- Wanaweza kusikia sauti 5-6 za Lingi

Kama mtumiaji amejibu hapana kwa swali mojawapo, inamaanisha hafaidiki vizuri na vifaa saidizi vya usikivu. Jaribu kutatua tatizo. Kama utatuzi huu hausaidii, muombe kuja kituoni ili akaguliwe afya ya masikio yake na kifaa chake. Kama suluhu ya tatizo haijapatikana, jadiliana na mshauri wa huduma na kama itahitajika ☞mpe rufaa kwenda kuonana na mtaalamu wa masikio na usikivu.

Elezea kwamba kila miaka miwili ni muhimu kukagua afya ya masikio na kurudia kipimo cha kusikia ili kuona kama kuna mabadiliko.

Kukagua kujua kama kifaa saidizi cha usikivu kinafanya kazi vizuri kwa kutumia bomba la kusikiliza. Kama kifaa saidizi kimoja au vyote viwili kwa pamoja havifanyi kazi, visafishe na badilisha vifaa saidizi ambavyo vimechakaa au kuharibika. Kama hii haitasaidia jadili na mshauri na itahitajika, kitume kwa mtengenezaji.

**Utunzaji na Ukarabati**

Utunzaji, ukarabati na utatuzi wa matatizo ni muhimu sana kwenye ufuatiiaji. Hii imezungumziwa sana kwenye moduli ya TAP kuhusu vifaa saidizi vya usikivu vilivyosetiwa tayari.

Hamasisha mlezi kurudi na mtoto kwenye kituo cha kutoa huduma muda wowote kama watapata shida kwenye kusikia au kutumia kifaa saidizi cha kusikia.